gaia

2024

# Kanuni za haki kwa Mazingira

## kwa Hatua ya Dharura kuhusu Taka na Methani



# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Sehemu ya 1. **Utangulizi** | 4 |
| Sehemu ya 2. **Kanuni za haki za mazingira katika sekta ya taka** | 6 |
| (1) Kuheshimu mipaka ya ardhi kuhakikisha kuna usawa wa mwingiliano | 6 |
| (2) Kuheshimu wanaokusanya taka na wafanyikazi katika sekta hiyo | 7 |
| (3) Kuimarisha ujumuishaji na kujenga mazingira ya uelewa kwa jamii | 8 |
| (4) Kuwajibika kuhusu uchafuzi wa hewa na uharibifu wa mazingira | 8 |
| (5) Kuunga mkono suluhu jumuishi kupitia kwa mabadiliko ya mifumo | 9 |
| Sehemu ya 3. **Utaratibu kwa watunga sera kuhusu taka na Kanuni za Haki kwa Mazingira** | 10 |
| Sehemu ya 4. **Muhtasari wa mwisho: Orodha ya hatua za kuchukuliwa kuhusu sera taka na tabia - nchi** | 20 |
| **Sisi ni nani?** | 24 |
| **Marejeleo** | 25 |
| **Kumbuka** | 26 |






Jose Luis Vargas/RADA

Sehemu ya 1.

# Utangulizi

## *Maono ya kuwa na mifumo ya mabadiliko kuelekea kwa kutumia bidhaa kikamilifu, haki kwa tabia-nchi, na hatua za dharura kwa methani*

- Katika kikao cha sabini na saba cha Disemba, 14, 2022, Baraza kuu la Umoja wa Mataifa liliidhinisha azimio la kutenga Machi 30 kuwa siku ya kimataifa ya kutumia kikamilifu bidhaa. Katika kutangaza maadhimisho haya ya mwaka, Umoja wa Mataifa ulitambua kuwa uendelezaji wa kutumia bidhaa kikamilifu utasaidia kufikia malengo na matarajio ya agenda ya 2030 ya maendeleo endelevu yanayojumuisha Lengo ya maendeleo Endelevu la 11 na Lengo la Maendeleo Endelevu la 12. Malengo haya yanazingatia mifumo yote ya taka, inayojumuisha taka za plastiki, hasara ya chakula na taka za vyakula , uchimbaji wa rasilimali ghafi na taka zinazotokana na vifaa vya elktroniki.
- Kutumia bidhaa kikamilifu inaelezwa kuwa uhifadhi wa rasilimali zote kwa jinsi ya kuzalisha kwa uzingativu, utumizi, utoshelevu, kutumia upya na urejeshwaji wa bidhaa, upakiaji, bila kuchoma vifaa, na pasi kuelekeza uchafu kwa ardhi, maji, ama hata hewani kwa jinsi ya kuhatarisha mazingira ama afya ya binadamu[1]. La muhimu zaidi ni kuwa mikakati ya kutumia biadhaa kikamilifu inazisaidia jamii kuzalisha na kutumia bidhaa wakati huo huo zikitambua uhaba wa rasilimali, mipaka ya ardhi na haki za jamii; mikakati hii muhimu inalenga kuendelea kupunguza kupotea kwa bidhaa kupitia kupunguza katika vianzo, ukusanyaji tofauti, kuweka takataka kwenye shimo na kuzitumia upya, kuhakikisha kuwa vifaa visizohitajika vimewekwa kwa hali safi na vinarejeshwa katika hali zao halisi ama vilivyotengenezwa viwandani. Desturi ya kutumia bidhaa kikamilifu ina maana ya kuwa na dunia ambayo bidhaa zote zinatumika kikamilifu, hakuna hasara inayotokea, na mahitaji ya watu – wafanyikazi na jamii – yanafikiwa kwa mfumo unaowalinda na huwezi kuharibu mazingira.
- Muhimu kujua usimamizi wa bidhaa zinazostahili kutupwa ni tatizo pana. Inahusiana na maeneo ya kisiasa, kitaasisi, kijamii, mazingira na uchumi. Hatua madhubuti katika sekta hii ya bidhaa zinazodhaniwa kuwa za hasara inatakiwa kuandaliwa kwa namna maalumu kwa kuzingatia sifa muhimu katika kila eneo. Inatakiwa kuchunguzwa ikiwa suala la moshi ya methani, uchafuzi wa hewa kutumia plastiki ama kuzuia chakula kupotea, na kushughulikia masuala hayo kikamilifu ina maana kutambua kuwa na mkakati wake wa kukabili tatizo la bidhaa hizo zinazodhaniwa kuwa mzigo.
- Kwa kuangazia uchafu unaotakana na methani haswa: sekta hiyo ya taka ni ya tatu kwa ukubwa kutoka uchafu unaotakana na binadamu wa methani, ambao upunguzwaji wake utaleta manufaa mengi ya haraka ya tabia - nchi kwa kuzuia kuchemka. Kiwango cha methani kilicho na uwezo wa kuteka joto ni zaidi ya mara 86 ya kaboni dioksidi kwa kipindi cha miaka kumi. Sekta ya taka inaweza kupunguza uchafuzi wa methani kwa asili mia 95 kupitia mbinu ya pamoja inayozuia hasara ya chakula, hurejesha chakula kingi kinacholika, ukusanyaji tofauti na kufanya mchakato wa taka zinazotokana na wanyama na mifugo na kupunguza uchafuzi katika maeneo ya kutupa taka. Utaratibu huu ni sehemu kubwa ya mfumo wa matumizi kikamilifu ya bidhaa.
- Sayari yetu na watu wanakabiliwa na matatizo mengi yanayoingiliana: utoaji na matumizi ya ekolojia ya ulimwengu na viwanja wa binadamu, kutokuwa na usawa kwa muda mrefu, athari inayotokana na kutokuwa na mwongozo wa kisheria kwa mashirika, ukosefu wa uwajibikaji na uwazi miongoni mwa makundi ya dunia yanayotoa maamuzi. Tunahitaji mabadiliko ya kuridhisha, kuondokana na mizozo hii katika njia iliyo sawa na kuwahusisha wengi, ili kubuni fursa za kazi na hakuna anayeachwa nyuma. Katika sekta inayolinda bidhaa kutopotea kwa vyovyote vile, haki kwa mazingira inajumuisha sekta ya jua kali ya kutumia bidhaa mara nyingi, kama vile wanaokusanya bidhaa ambazo hawataki kupoteza kiwango chochote, jamii zilizofaidi na vifaa vya kuhifadhi bidhaa zilizotumika kama vile mashimo ya kuhifadhi taka, na jamii ambazo zina matatizo makubwa na zimelemewa na athari ya uchafuzi wa hewa, kama vile wanawake, watoto, wazee, jamii ambazo zina mapato ya chini, watu wasiokuwa wazungu na kadhalika. Bila shaka ni muhimu kuchukulia mazingira kama eneo la haki, kukubali kwamba kuna kutegemeana kati ya jamii, wanyamapori na mfumo wa ekolojia, kwani ilitambuliwa awali na Katiba ya Ecuador mwaka 2008.
- Historia inatufundisha kuwa ukosefu wa haki za mazingira unatokana na mifumo ya matumizi mabaya lakini huwa yanaorodheshwa kuwa tatizo linaloweza kutatuliwa kiufundi ama kifedha. Badala yake ni muhimu kutafuta mbinu ya kutoa haki kwa mazingira kwa misingi ya kanuni za binadamu, siasa, uchumi na haki za kitamaduni; usambazaji wa demokrasia; na uwajibikaji katika usimamizi.
- Suluhu zinazoruhusu matumizi kamilifu ni msingi muhimu katika juhudi za kupunguza gesi chafu kutoka kwa kivungamea na kujenga uthubutu na suluhu kwa mabadiliko ya tabia -nchi na kuhakikisha kuwa kuna haki, usawa na mambo mengine. Mwito huu wa dunia wa haki kwa mazingira ni mpana na unatilia maanani mseto wa watu na tamaduni pamoja na haki za binadamu katika kushiriki katika michakato ya siasa ambayo hujenga, kudhibiti na kutekeleza sera ya mazingira . Kuwepo kwa sifa na kanuni hizi inaonyesha mshikamano wetu kwa makundi ya dunia kuhusu mazingira na haki kwa tabia - nchi, na mapambano ya jamii zilizotengwa na kuhakikisha kuwa zinapata haki zao za kuwa na mazingira safi na salama.



Rommel Cabrera/GAIA



Polis Institute

Sehemu ya 2.

# Kanuni za haki za mazingira katika sekta ya taka

## *Kanuni tano zinazotoa mwongozo wa kuchukuliwa hatua*

### 1.
### KUHESHIMU MIPAKA YA ARDHI KUHAKIKISHA KUNA USAWA WA MWINGILIANO

**Kutambua mipaka ya ekolojia, viwango vya taka vinatakiwa kutumika kwa mujibu wa mabadiliko ya tabia - nchi na kuelekeza mabadiliko yanayofaa kuhakikisha kuwa kuna usawa wa vizazi.**

Kutunza vizazi vijavyo' haki kwa mazingira bora inahitaji kuheshimu mipaka ya ardhi iliyowekwa. Binadamu wakati huu wanavuka mipaka stahiki, mpango ambao unatakiwa kugunduliwa na kubadilishwa ili kuzuia matatizo ya dharura ya tabia - nchi, kupungua kwa bionui na kumalizika kwa baadhi ya viumbe ambavyo havileti uimara katika dunia. Hatua ya kukumbuka kushughulikia mipaka ya ardhi na haki kwa mazingira inadhihirisha haki kamili kwa kila mtu, haswa walio katika hatari ya kupata maji, chakula, kawi na mazingira safi. Mabadiliko ya haki ya kuleta usawa wa vizazi na utoshelevu unahakikisha kuwa matumizi ya rasilimali, kulinda hali ya kila mtu, inajumuisha hata vizazi vijavyo na wakati huo huo kupunguza masalio ya kaboni.



Katika muktadha huu, mchango wa sekta ya bidhaa zilizotumika na kutoa masalio kwa mazingira na uharibifu wa tabia - nchi ni muhimu na wa dharura, na unahitaji kufuata yaliyo muhimu ambayo yametambuliwa na viwango vya bidhaa hizo zinazozuiwa kupotea – hii inamaanisha kuzuia kupotea kwa bidhaa na kutumia kikamilifu bidhaa zinazotakiwa kupotea kwa jinsi bora zaidi na kuondoa kwa awamu matumizi ya teknolojia za kuzika taka kwa ardhi na kuchoma.

Kanuni hii inahusisha serikali, taasisi za umma na binafsi zinazotakiwa kuwa na mbinu ya kujifanyia mageuzi na kuelekeza nguvu zao kwa utoshelezaji na kubadilisha mwenendo ulioenea wa kutumia kupita kiasi bidhaa za kawaida. Zaidi ya hayo taasisi zinatakiwa kuondoa vikwazo vya matumizi, mbali na kuimarisha na kuwekeza kwa watu binafsi na wanafamilia watumizi kuwajibika na kuzingatia ruwaza za matumizi.

### 2.
### KUHESHIMU WANAOKUSANYA TAKA NA WAFANYIKAZI KATIKA SEKTA HIYO

**Kuhifadhi na kuimarisha haki za binadamu, tunatakiwa kuzingatia usawa na haki katika yote tunayofanya, kulinda maisha ya wanaokusanya taka wafanyikazi katika sekta hiyo ya taka kuhakikisha kuwa kwanza hawapati madhara yoyote.**

Sera zinazohusika na usimamizi na utakelezaji wa miradi ya taka inatakiwa kuendana na mwelekeo wa kutokuwa na madhara yoyote, kumaanisha kuwa athari kwa makundi yaliyokuwa katika hatari ama jamii zilizotengwa zimetembuliwa, kupuuzwa ama kushughulikiwa. Jamii hizi hazitakiwi kuwa katika hali mbaya mno kutokana na athari za sera za au miradi kuhusu bidhaa zinazotakiwa kutupwa. Mbinu hii inahusisha kutambua haki za kisheria, kijamii na maadili na kutathmini hatari zinazozowakabili washikadau wote na haki zao, uzingativu mkubwa ukiwa kwa jamii ambazo hazijiwezi. Msisitizo ni kuwa haki za msingi za utambulisho zinatakiwa kutambuliwa na kwa wanaokusanya taka na wanaofanya kazi katika sekta hiyo. Wanaofanya kazi hizo za kukusanya masalio taka wanatakiwa kuwa salama, na kwa mazingira bora ya kazi bila kulazimishwa kuchagua kati ya kufanya kazi hatari kwa afya yao na kukosa ajira.




Mataifa na serikali katika ngazi zote zina jukumu kuwalinda watu wake na makundi dhidi ya haki zao kudhulumiwa. Ni muhimu kutambua mila na desturi za jamii zote na kutoa nafasi sawa kwa wote kufikia rasilimali, kutoa huduma za msingi kama vile chakula na makazi kwa wote. Kulinda haki asilia wa watu asilia kujitegemea kunatakiwa kuzingatiwa. Hii inatakiwa kujumuisha mwonekano wa athari zilizopatikana kwa pamoja zinazotokana na vifaa vingi vinavyochafua hewa na mchango wake kwa jamii zilizolemewa na mizigo (Wakati mwingine inajulikana kama "Maeneo yanayopuuzwa"). Jamii zilizobebeshwa mizigo kwa kiasi kikubwa zimo katika hatari ya ubaguzi wa haki kijinsia na dhuluma ambazo zinatakiwa kuondolewa.

# 3.

## KUIMARISHA UJUMUISHAJI NA KUJENGA MAZINGIRA YA UELEWA KWA JAMII

**Katika mchakato wa kutoa maamuzi, kuimarisha ujumuishaji na kuhusika katika kiwango kinachoridhisha ni lazima, pamoja na kujenga uelewa katika jamii ya mashinani na utaalamu.**

Sera na utekelezaji wa miradi inayohusiana na usimamizi wa taka, rasilimali inatakiwa kuhakikisha kuwa kuna ujumuishaji unaonekana, usawa katika kuhusika katika haki zote za wadau, kuanzia katika kupanga maendeleo katika kipindi chote cha mradi. Michakato huru wa awali unaotoa ruhusa inatakiwa kudumishwa kwa wale wanaokusanya taka, wale wanaofanya kazi katika sekta ya taka na jamii zinazotenganishwa na umma ili zihusishwe katika kila hatua ya maamuzi ikijumuisha kutathmini kwa mahitaji, kupanga utekelezaji, kuzingatia sheria na kuweka katika mizani. Panatakiwa kuwepo na juhudi za ziada kuwezesha usawa katika kuhusika kwa makundi yaliyotengwa kwa misingi ya (wala si kujikita tu katika) rangi, kabila, tabaka, jinsia, ulemavu, na kadhalika. Si hayo tu, sera ya umma inayoathiri usimamizi wa taka, inatakiwa kutambua na kuhusisha



utaalamu wa makundi yanayopatikana hapo na washiriki ambao wanajumuisha pia sekta ya Juakali. Sera hizo zinatakiw akuongeza dhamana katika kazi iliyofanywa awali katika eneo hilo wala si kwa dhamira ya kuvuruga uchumi uliopo katika sehemu hiyo. Usimamizi wa taka unatakiwa kuridhisha jamii ya mahali hapo, kuwa na athari ndogo, kwa kiwango kidogo, iliyosambazwa, inayoweza kukidhi tabia - nchi, na jamii zote zinatakiwa kuwezeshwa kupata teknolojia, ujuzi na maarifa.

# 4.

## KUWAJIBIKA KUHUSU UCHAFUZI WA HEWA NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA

**Uchafuzi wowote wa hewa na uharibifu wa mazingira unatakiwa kushughulikiwa kwa uwajibikaji, kuweka utaratibu wa kufidia na kuzuia madhara.**




Mashirika binafsi na wengine ambao wamekuwa wakiwadhuru watu ama mazingira kupitia kwa sera na miradi ya taka wanatakiwa kuwajibishwa. Jamii zilizoathiriwa zinatakiwa kuwezeshwa kupata haki, fidia, afya bora na urejesho wa maisha yao wakati wanapodhurika, na kuhakikisha kuwa vigezo vinavyotumiwa ni vya kimataifa. Sera zinazoongoza zinatakiwa kuandaliwa kwa jinsi ya kudhibiti nguvu za mashirika na kuzuia uhalifu zaidi katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Katika hali hii, ni muhimu kuzingatia kanuni ya ukaribu,: usimamizi wa taka unatakiwa kuwa karibu sana na eneo la uzalishaji na kusafirisha taka kwa mataifa ambayo hayana mifumo thabiti ya usimamizi wa taka ama sheria na kanuni za mazingira — inayojulikana kama ukoloni wa taka — hii inatakiwa kukoma.

Mchafuzi anatakiwa kutozwa faini kubwa, kwa kuzingatia sheria ya kimataifa ya mazingira, imewekwa hapo ili kuhakikisha kuwa kundi linalohusika na uchafuzi (kwa vitendo ama matukio) linagharamika kwa sababu ya kusafisha. Hata hivyo ili kufanikisha mkakati huu, gharama inatakiwa kuwa ya juu zaidi na tofauti kwa lengo la kuzuia kuendelea kwa uchafuzi wa mazingira. Msimamo huu kwa vyovyote vile hutakiwi kuchukuliwa kama haki ya kuendelea kuchafua hewa hata ikiwa faini zinalipwa.

Mbinu za kuzuia na kuchukua tahadhari zinatakiwa kutumika. Ya kwanza ni kushughulikia hatari zinadhihirika, huku ya tahadhari ikijikita katika sayansi isiyotabirika. Ikiwa kuna tishio la madhara kwa watu ama dunia, basi ukosefu wa sayansi kamilifu huwezi kutumiwa kuchelewesha masharti ya gharama inayoridhisha kukomesha madhara hayo.

# 5.

## KUUNGA MKONO SULUHU JUMUISHI KUPITIA KWA MABADILIKO YA MIFUMO

**Mfumo maalum unatakiwa kutumiwa ili kupata suluhisho kwa migogoro iliyopo kama vile tabianchi, afya ya umma, njaa, jinsia, ubaguzi wa haki kwa rangi na kitabaka, mizozo na vita na kuhakikisha kuwa sulu hizo katika sekta ya taka inafikia na kupita Malengo ya Maendeleo Endelevu na dhamira za tabia - nchi.**

Sera na utekelezaji wa miradi na taka na usimamizi wa rasilimali inahitaji kuratibiwa, kutengenezwa na kutathminiwa kutoka kwa mwonekano wa mfumo, kuhakikisha kuwa inaingiliana na faida za mazingira, kijamii na kiuchumi. Suluhisho haliwezi kupatikana tu kwa kuegemea hatua iliyochukuliwa kwa upande mmoja. Kwa kuchukua hatua yoyote ya tabia -nchi kabla ya kuelewa kikamilifu namna ya kuzuia matatizo, hatua za uasilishaji na maendeleo endelevu hupatana na kuimarishana, inaweza kuwa hatari na kuharibu chanzo halisi cha mabdiliko ya tabia - nchi. Katika dunia iliyoathiriwa na umasikini, njaa, kutokuwa na usawa wa jinsia, vita na mabadiliko ya tabia - nchi, usimamizi wa mifumo ya taka unatakiwa kuimarisha na kuambatanishwa na mfumo wa malengo makubwa, kutambua kutegemeana kati ya binadamu wote katika dunia, kuthamini na kutambua kazi ya utunzaji na kuhakikisha huduma za msingi kwa umma kama vile maji, afya, kawi, elimu, chakula na kadhalika vinatolewa kwa wote.

Juhudi za kuingilia kati zinatakiwa kuunga mkono mahitaji ya kiekolojia ya sera za mjini na mashambani za kusafisha na kujenga upya maeneo yetu ya mijini na mashambani kwa kusawazisha uhalisia na ekolojia, kujiepusha na uharibifu wa hewa yenye sumu, na kubuni mazingira safi ya kutumia upya na kutumia kwa mara nyingine, kurejesha madini kwa michanga na bidhaa kwa jamii, kulinda ubionui na kupanga upya utegemeaji baina ya wanyama na dunia. Mikakati hii chini ya mwavuli ya maono ya kutumia bidhaa kikamilifu kadhalika una manufaa kama hewa safi, maisha yaliyoboreshwa, utoshelevu wa chakula miongoni mwa mambo mengine, ambayo jamii zinatakiwa kupata bila ugumu haswa zile ambazo kwa wakati huu zimeathiriwa na uchafuzi wa mazingira.

Mtazamo wa mfumo unamaanisha pia kupanga upya bidhaa na kuziweka pamoja isipokuwa vifaa vya sumu, na kuhakikisha kuwa mpangilio wa matumizi yanazingatia afya njema kwa watu na dunia, na kuratibu haki ya kurekebisha na kupiga marufuku vitu visivyokuwa na manufaa ambavyo utekelezaji wake unafanywa na kampuni zinazotaka kupata faida zaidi. Mkondo uliopangwa pia unatambua kwamba kuna deni la ekolojia kutoka sehemu za kaskazini hadi kusini mwa dunia, na kwamba sera za usimamizi wa taka na miradi hazitakiwi kuimarisha ukosefu wa usawa na haki uliopo duniani





Sehemu ya 3.

# Utaratibu kwa watunga sera kuhusu taka na Kanuni za Haki kwa Mazingira

Seoul KakaoTalk

***Kanuni za haki kwa mazingira katika sekta ya taka ambazo zimeorodheshwa hapo juu inatoa fungu la vigezo na mbinu za mchakato wa kutoa maamuzi katika uwanja huu. Ili kanuni za taka na mazingira kutimiza malengo yake, panahitajika sera bora ya mazingira pamoja na mfumo bora wa utekelezaji. Licha ya hayo, ni muhimu kuwa na mpangilio mwafaka wa utekelezaji na kisanduku cha hifadhi kuhakikisha kuwa hakuna kinachopotea pamoja na kuwa na mikakati ya kupunguza methani.***

***Yafuatayo ni mapendekezo kuhusu namna watunga sera wanaweza kutekeleza kanuni hizi. Mwongozo huu ni kwa watunga sera, wataalamu kuhusu uendelevu, wanaharakati wa mazingira na waandalizi wa mashinani wanaolenga kupunguza methani katika juhudi za kutumia bidhaa kikamilifu na haki kwa mazingira. Kimsingi, kanuni hizi zinatakiwa kutengenezwa na kutumika katika muundo fulani, ustawishaji na utekelezaji wa sera ya mazingira na taka katika viwango vyote***

## 1. Kutumbua mipaka iliwekwa na kuelekea kwa utoshelezi

**Ili kutambua mipaka ya ekolojia, tunatakiwa kufuata ngazi za taka kugeuza mabadiliko ya tabia – nchi na kusambaratika kwa mazingira hadi kwa utoshelezi.**

Viwango vya taka — jinsi imeelezwa hapo chini — inatoa mwongozo kwa sera zinzohitajika kushughulikiwa kwa dharura kuingiliwa kati katika sekta ya taka. Kilele hapa ni kuzuia taka katika mpangilio huo wa taka katika kiwango cha juu, na mara nyingi inahusisha kundi la sera ambazo zinapatikana nje ya maeneo maalum ya usimamizi wa taka

Kuzuia hasara ya taka kunahusisha kupunguza uzalishaji wa bidhaa zinazostahili kutupwa , zinatengenezwa upya ili zitumika kikalifu na matumizi yake kurudiwa tena ili kuwezesha utumizi mdogo wa rasilimali zinazotumika kwa jumla. Kwa njia hii, sera za kuzuia uharibifu zina manufaa kwa kulinda mabadiliko ya tabia- nchi na kuasilisha, na kuchangia kwa lengo la utoshelevu: na kusimamia mahitaji ya kimsingi na ufanisi kwa wote bila kuwa na upungufu au uziada, na kuwekeza vizuri katika mifumo kutumia tena huku kukiwa na upunguzaji na kujiepusha na matumizi kupita kiasi, haswa kwa bidhaa ambazo zinatumika tu mara moja.

Sera kuhusu kuzuia taka inatakiwa kumaliza mipango isiyokuwa na maana na kuwapa watumizi haki za kurekebisha badala ya kufikiria jinsi ya kuacha na kununua bidhaa mpya; inahitaji betri za kuondolewa ama kubadilishwa, kujiepusha hali ya kutoingiliana na zanatepe na zanamango, kuratibu haki za kukarabati mabaki yanayotokana na vifaa vya elektroniki na kadhalika.

Vifaa vyote vya sera vinaweza kuwa na athari kubwa kuhusu kuzuia kupotea kwa bidhaa, ambayo ni muhimu mno inapokuja kwa hasara ya kupoteza chakula na mabaki yanayotokana na chakula. Cha muhimu kutaja ni kuwa kuna ongezeko la kilimo halisi mitandao ya kuhifadhi taka imepangwa katika miji ili kukusanya kinyesi na kuhakikisha usimamizi unakuwa wa jamii na unasambazwa. Shughuli hizi zinatoa kipau mbele kurejesha chakula katika hali bora kwa hifadhi ya vyakula, kuwalisha mifugo, na kusambaza huduma za kutupa taka. Mipango hii inatakiwa kuwekezwa na kufanywa tena katika utaratibu ufuatao:

1. **Kuandaa na kuasilisha mpango kamilifu kwa lengo la kupunguza kupotea kwa mabaki ya vyakula katika sehemu ya mabadiliko mapana wa mfumo endelevu wa chakula[2];**
2. **Chochea mfumo wa kawaida wa chakula kupitia kwa kilimo kinachoungwa mkono na jamii na mipango ambayo itazuia kupotea kwa chakula katika kiwango cha msingi;**
3. **Kujenga mazingira ya kawaida ya chakula na kuhamasisha kwa upana washirika kutoka sekta binafsi na umma kuzindua mpango wa kuzuia shughuli za kupotea kwa mabaki yanayotokana na chakula;**
4. **Kuimarisha kampeni ya uelewa na elimu kuhusu thamani ya chakula kupitia kwa mpango wa elimu ama kampeni madhubuti zitakazowachochea raia kupunguza kupotea kwa mabaki ya chakula;**
5. **Kubuni mfumo bora wa usimamizi wa taka za bio kuhakikisha mabaki yanayotokana na chakula yanabadilisha na kuwa mbolea ikiwa hali hiyo haiwezi kuzuiwa.**

Utekelezaji wa kanuni hii unaonyesha kujitolea binafsi kwa mabadiliko ya kitaasisi kwa kuzingatia mipaka ya ekolojia iliyowekwa. Mwanzo ujenzi na utekelezaji wa sera za taka na tabia - nchi itahitaji kila mara mafunzo na ufundi wa kutosha kwa mamlaka za vijijini na mashirika katika ngazi za mashinani.

Kisha taasisi zinatakiwa kufuata protokali na desturi za kijani na uendelevu na utoshelevu, kuondoa vikwazo vya kupunguza matumizi, na kuimarisha na kuwawezesha watu binafsi na familia watumizi kufuata na kuwajibika pamoja na kujali mipangilio ya matumizi.

Sera maalum za ununuzi wa nyenzo za kijani zinahitajika katika hafla binafsi za taasisi, kama vile sahani zinazotumiwa zaidi ya mara moja mezani, kutumia samadi katika maeneo ya kijani, kujiepusha na plastiki inayotumiwa mara moja tu kudhibiti hasara inayotokana na chakula, na kadhalika. Taasisi zitakiwa kuwa mfano wa kuigwa na muundo wa mabadiliko ya utamaduni na kuelekea katika uendelevu na kuheshimu rasilimali chache zinazopatikana kwenye ardhi.



Zero Waste Durban

# Viwango vya taka zinazotokana na mimea na wanyama kupunguza Methani katika Sekta ya Taka kwa kuzingatia kanuni na Maadili ya Haki kwa Mazingira

1. **Uzuiaji wa taka zinazotokana na wanyama na mimea: mbinu zilizopo katika kila hatua ya mfumo wa kusambaza kutoka kwa uzalishaji, usafirishaji hadi kwa matumizi**

- Kuzuia taka ndiyo mkakati muhimu wa kupunguza methani katika katika sekta ya taka; kila tani moja ya taka inayotokana na wanyama ama mimea na haipitii mkondo wa taka inakwepa methani na inaweza kuzalishwa kwa kuzika taka kwa ardhi mbali na moshi chafu unayotokana na uzalishaji na usafiri.
- Kupotea kwa chakula na hasara inayotokana na hilo inachukua asili mia 10 ya hewa yote chafu ya gesi ya kivungamea kote duniani na kiwango kikubwa cha mabaki ya hewa chafu ya Methani ni hali inayostahili kuepukwa. Zaidi ya hayo kuna fursa ya kuzuia mabaki ya chakula na hasara inayotokana na chakula katika kila hatua zinazopitia bidhaa asilia, kwa kubadilisha misaada inayopendelea uzalishaji maradufu wa vyakula na kuweka mpango wa kuzingatia uhitaji ama wajibu wa utoaji wa msaada wa vyakula kwa maduka makubwa, kuelimisha wateja kuhusu kuzuia kupotea kwa mabaki yanayotoka kwenye bidhaa.[3,4] Sheria ya hivi majuzi ya Ufaransa ya kuzuia kupotea kwa cha chakula, kwa mfano inapiga faini maduka makubwa ambayo yanazidisha kiwango kilichowekwa kwa vyakula vinavyoweza kutupwa.[5]

2. **Utoshelevu wa chakula: kusambaza tena kwa watu na kuibadilisha kuwa bidhaa za kuhifadhi chakula**

Panaposhindakana uzuiaji wa mmoja kwa moja, juhudi huelekezwa kwa njia bora mbadala ya kupata tena – masalio ya chakula yanaweza kuelekezwa kwa watu wenye uhitaji na kutengenezwa ili itumike na kuwa bidhaa kama vile jemu. Ushirikiano kati ya hifadhi za vyakula, maduka ya kuuza vyakula katika serikali za miji huko Milan, Italia kwa mfano imeokoa zaidi ya tani milioni 130 za vyakula kuharibika kila mwaka katika miaka mitatu, na kuweka jiji hilo kufikia kiwango inacholenga cha asilia mia 50 ya kupunguza hasara kwa vyakula kufikia 2030.[6,7] Kuzuia kupotea kwa chakula na mabaki, inajumuisha kupigia debe mipango inayotoa nafasi ya kupatikana kwa




Source: Institute for Local Self-Reliance

chakula kilicho na madini toshelevu kwa watu walio na umasikini mkubwa na kuwa na chakula toshelevu ni kupiga hatua kubwa mbele.

3. **Kupata tena taka inayotokana na chakula: Kusambaza tena chakula kwa wanyama**

Kutenganisha mabaki katika vianzo na ukusanyaji tofauti ni sera ya msingi inayoamua ubora wa jinsi ya kutumia mabaki ya chakula na utendaji mwingine wa kiwango cha juu kama ilivyoelezwa hapo chini. Mfano mkubwa wa sera ya kutenganisha mabaki ni marekebisho ya 201 ya mwongozo wa agizo la Jumuiya ya Ulaya ambayo imetoa malengo chanya kuhusu usimamizi wa taka zinzotokana na mimea na wanyama katika nchi zote 27 za Jumuiya ya Ulaya. Agizo la jukumu la kukusanya tofauti taka zinazotokana na mimea na wanyama zote kufikia mwisho wa 2023 imechangia mafanikio makubwa katika ukusanyaji tofauti wa viwango na Jumuiya ya Ulaya inapanga kuasilisha malango ya ziada ya kupunguza uharibifu wa vyakula kwa zaidi ya asili mia 50% kufikia 2030 na kujenga malengo yanayofungamana na sheria kuhusu kupunguza kuharibika kwa vyakula.[8,9]

Hata kunapokuwa mipango ya maalum ya kuzuia taka, kuna baadhi ya taka zinazotokana na wanyama au mifugo bado zitazalishwa. Katika hivi vifaa vilivyotupwa, kuna kutenganishwa kwa vianzo – ambapo mbolea iliyotupwa natenganishwa na taka nyingine katika wakati wa uzalishaji (nyumbani, biashara na kadhalika) – ni muhimu. Vianzo- Taka inayotoka kwa wanyama na mimea inatakiwa kukusanywa tofauti, kuhakikisha kuwa kuna mkondo safi wa bidhaa za taka na mbinu za kushughulikia mfumo huo wenye athari kubwa kama vile kuhifadhi taka, kuhifadhi taka na kusaga uchafu na taka na uelekezaji wa chakula cha wanyama ambao unaweza kufanyiwa katika eneo hilo, katika sehemu zilizo za vifaa vya kuhudumia jamii, ama kuwa na sehemu moja kuu na kuweka vifaa kwa kutegemea mahitaji na uwezo walio nao watu wa mashinani.

Kadhalika, kutumia masalio ya taka kuwalisha mifugo kunazuia moshi ya methani kutoka kwa taka zilizozikwa kwa ardhi na inaweza kuiondoa katika sehemu yake, vyakula vya mimea vinavyozalishwa na kawi toshelevu (Tazama sehemu ya 2). Japokuwa makadirio yanaonyesha uwezekano wa kupungua kwa methani kwa kutumia taka kwa chakula cha wanyama haupo, tathmini kuhusu mzunguko huu inaonyesha kuwa desturi hiyo inaweza kuleta matokeo makubwa ya kupunguza gesi ya kivungamea badala ya kuhifadhi taka ama kuhifadhi taka na kussaga uchafu na taka.[10,11]

4. **Kutumia upya vifaa: Kuhifadhi taka na kusaga uchafu na taka inayotokana na wanyama ama mimea**

Hifadhi ya taka: Tofauti na kujazwa taka katika ardhi usimamizi bora wa shughuli za taka hutoa viwango vidogo vya methani ambayo huwa imeharibiwa na viini vya bacteria.[12,13,14] Uhifadhi wa taka unaweza kuzuia zaidi ya asili mia 99 ya hewa chafu ya methane ambayo ingeweza kutolewa kutoka kwa mashimo ya ardhi yaliyojazwa, na kupunguza kwa kiasi kikubwa hewa chafu katika sekta ya taka. Kusambaza usimamizi katika maeneo ya kuhifadhi taka ni jambo lililozingatiwa lakini kuna hifadhi nyingine na jinsi tofauti katika miktadha yote.[15]



Rommel Cabrera/GAIA

Kusaga uchafu na taka zinazotokana na wanyama au mimea : ambapo taka zisizohitajika zinasagwa kwa makusudi bila oksijeni kuzalisha methani kwa mafuta – inaweza kutoa usaidizi ama kuwa njia mbadala ya kutupa taka. Tofauti na kuzika taka katika ardhi, ambazo mara nyingi huvuja methani katika anga, vifaa vya usagaji huu ni vyombo vinavyoukusanya methani hadi ichomeke na kuwa mafuta na kuibadilisha na kuwa biojeni. Usagaji huu wa uchafu na taka zinazotoka kwa wanyama na mimea pia inazalisha sehemu ndogo ya taka na inaweza kuhifadhiwa na kutumiwa kubadilisha udongo. Mbinu hii ya kusaga uchafu na taka za mimea na wanyama inatumika zaidi katika maeneo yenye idadi kubwa ya watu na kiwango kikubwa cha taka na hamna vifaa vya kuhifadhi taka ama mabaki lakini ina gharama kubwa ya mtaji na inahitaji mafunzo ya kitaalamu kuendesha shughuli hiyo.[16] Vifaa vya kusaga uchafu na taka za wanyama vya bei nafuu na viwango vidogo vimekuwa vikitumika kwa mafanikio makubwa mno katika sehemu za mashambani ambapo ni vigumu kupata kawi inayorisha katika nchi kama vile Bangladesh, India na Uchina.[17]

Hata hivyo ni muhimu kutambua athari zilizo mbele zinazokabili mapungufu ya usagaji uchafu na taka za wanyama na mimea kama vile kuzika taka kwenye ardhi na kuharibu gesi ya bio badala ya kuitumia kama mafuta, kuteketeza kawi asili na kuzidisha halijoto, kuponda upya, mimea ya kilimo kupitia kawi toshelevu badala ya taka zilizotupwa na kudhaniwa kama ushindani wa kweli kati ya kawi ya upepo na kawi ya sola. Ni muhimu pia kuhakikisha matumizi bora ya vifaa vya kusaga uchafu na taka za wanyama na mimea. Ni muhimu pia kuhakikisha kuwa utendakazi wa vifaa vya kusaga na mzuri ili kufikia utoshelevu wa kifedha na kuzuia uvujaji wa methani kwa anga baada ya uzalishaji. Kusaga uchafu na taka katika sekta ya kilimo inaweza kuwa kivutio kikubwa cha kuzalisha mbolea ya wanyama na taka nyingine na kufifisha fursa nyingine kama vile kupunguza kupotea kwa taka na kuhifadhi taka.[18] Hivyo basi kusaga uchafu na taka za wanyama na mimea, kunaweza kufanya kazi vizuri mkumbo wa mabaki ya mbolea kutoka kwa wanyama katika baadhi ya maeneo ambayo yanajitosheleza vizuri kiutendaji lakini sawa tu na uhifadhi wa taka, inatakiwa kujumuishwa katika mfumo mzima wa kutumia bidhaa kikamilifu kwa jumla ambao unatilia maanani zaidi uzuiaji.

5. **Kutumia bio kuimarisha mabaki ya takas**

Kwa misingi kuwa baadhi ya uchafu kutoka kwa mifugo na mimea itasalia kuwa katika mikondo ya mabaki ya taka hata baada ya kutenganishwa katika vianzo na kushughulikia taka hizo, taka za mabaki hazitakiwi kuzikwa kawa ardhi kwanza kabla ya kupitia ustawishaji wa kibiolojia. Hii inaweza kujumuisha kuchanganya kusikokuwa na utata na mbinu za kupitisha hewa katika mseto wa mchanganyiko wa majimaji ama urejesho wa bidhaa changamano na uchunguzi wa mifumo ya kibiolojia. Katika njia hii, uimarishaji wa bio unatoa uchunguzi wa mwisho kwa vifaa vya taka, vinavyojumuisha kuharibika ama "kuchafuka" kihalisia itasalia katika mkondo wa mabaki ya taka.

**6. Urekebishaji: Sehemu ya juu iliyo hai kibayolojia na gasi inayotekwa kutoka kwa taka zilizozikwa kwa ardhi – unatakiwa kuwa uamuzi wa mwisho kuuelekeza**

Hata baada ya kuwa na mabadiliko kamili ya kihalisia hufikiwa, moshi ya methani unaoendelea kutoka kutokana na taka zilizozikwa katika ardhi zamani bado suala hilo litaangaziwa na maeneo kulikozikwa taka yataendelea kutoa methani kwa miaka bada kukataa kukubali taka mpya.[19] Kwa bahati nzuri ardhi ambayo taka zinazidi kuzikwa ndiyo inayochangia moshoi mwingi kutoka katika ardhi kulikozikwa taka japo zimefungwa,- inajulikana kama moshi wa kale – inawakilisha tu karibu 9% ya tatizo.[20] Uwanja unaopanuka wa utafiti unapendekeza kuwa sehemu ya juu ambayo ni hai – ngazi ama vifaa vya taka juu ya ardhi ambako kumezikwa – inaweza kupunguza moshi kwa kiasi kikubwa. Kwa kujenga jamii yenye viini ambavyo vinasaga methani na inapanda kutoka chini ya ardhi kulikozikwa taka, sehemu hai inayofunika inaweza kupunguza moshi wa ardhi kulikozikwa taka kwa asilimia 63 kwa wastani.[21,22,23,24] Kwa kutegemea hali ya mazingira inaweza kutoa moshi "hasi" kwa kuvuta methani kutoka kwa anga.[25,26] kwa upande mwingine, msaada wa kifedha kwa sehemu hai inayofunika inaweza kusababisha hasara kubwa ya kutupa taka ya kiwango cha chini chini ya ardhi kunakozikwa taka kama mkakati wa kuokoa hali, ambayo inatakiwa kuepukwa.

Njia ya mwisho ya urekebishaji wa moshi wa methani – ambayo inatakiwa tu kutumika baada ya utekelezaji wa mikakati ya kutumia bidhaa kikamilifu – inateka gesi kutoka ardhi kulikozikwa taka. Katika mchakato huu, mapbomba huwekwa katika ardhi kulikozikwa taka ambayo inaruhusu gesi, ambayo inawakilisha asilimia 35 – 50 ya methani,[27] inatakiwa kukusanya na kupitishia kwa mabomba katika ardhi. Kutoka hapo inaweza kupanuliwa ama kuchomowa kuzalisha kawi, na kuifanya methani iliyopo kuwa Kaboni dioksidi. Unasaji umadhubuti unaweza kuwa na tofauti kubwa, hata hivyo kuwa na 10–65% ya methani inayolengwa kukwepa had kwenye anga[28] na ziada ya moshi unayotoka kwa mabomba yaliyovuja na muundo wa kusafirishia.[29,30] Utekaji wa gesi inayotoka katika taka zilizozikwa kwa ardhi ina kaboni nyingi kupita taka kwenye shimo na kusaga uchafu na taka zinazotokana na mimia na wanyama kunatakiwa kufanywa kwa tahadhari. Katika visa vingine, uwepo wa fedha wa kukusanya gesi hiyo umechochea kampuni za usimamizi wa taka na manispaa kuelekeza mabaki ya taka katika miradi mingine (kama vile chakula cha wanyama kuhifadhi taka) kurejeshwa katika mfumo wa kuzika taka ardhini kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo.[31,32]

**7. Haikubaliki kamwe: kuchoma, kusaidiana kuchoma na njia nyingine za kupima matumizi ya gesi**

Kuchoma hakutakiwi kutumiwa kudhibiti mabaki ya taka. Kuchoma huchafua zaidi hewa, kuna gharama kubwa na kaboni nyingi, ina gharama kubwa ya mtaji na matumizi makubwa ya fedha za kuendesha mradi huo unaosimamia udhibiti wa uchafuzi wa hewa, kuchunguza kiwango cha hewa, usimamizi wa majitaka na utupaji wa majivu.[33] Gharama hizi kubwa hufanya maeneo haya ya kuchoma kufungwa na yamefilisi bajeti za manispaa kwa mamilioni ya fedha na hata kufika dola bilioni moja za Marekani kwa baadhi ya matukio ukilinganisha na kuhifadhi taka ambako kuna gharama ndogo ya usimamamizi pamoja na gharama ndogo za mtaji.[34,35,36] Kuchomwa pia kuna hadhi ya ya chini mno katika mtazamo wa tabia – nchi. Ingawa inaweza kuokoa mvuke wa methani kutoka kwa mabaki ya taka, inazalisha viwango vikubwa vya kaboni diokside wakati plastiki na vitamba visikokuwa asilia vikichomeka katika mseto wa taka za manispaa.[37] Inapotumiwa katika uzalishaji kawi, kile kinachoitwa "kutoka taka-hadi-kawi" matanuri hutoa moshi zaidi kwa kila fungu la kawi linalozalishwa kushinda chanzo kingine chochote cha kawi.[38] Hatimaye bidhaa za taka zinazotoka kwa wanyama na mimea katika masalio ya taka si ridhishi kwa mtazamo wa mwendeshaji shughuli hiyo kwa sababu taka zinazotoka kwa wanyama na mimea zina unyevu mwingi na hupunguza kiwango cha joto kinachopatikana na kuzalisha zaidi maeneo ya kuchafua hewa ambayo yanatakiwa kudhibitiwa kwa vyovyote vile. Kutokana na sababu hizo, kutofautisha chanzo na kushughulikia mabaki ya taka ndiyo njia bora ya kuteka ya kunasa gesi inayotoka katika taka zilizozikwa ardhini na uchomaji.

*Rommel Cabrera/GAIA*




# 2.

## Heshima kwa wote wanaokusanya taka na wanaofanya kazi katika sekta ya taka

**Ili kudumisha na kuimarisha haki za binamu, tunatakiwa kuzingatia usawa na haki katika vitendo vyetu, kutimiza mabaliko ya kweli, kulinda, maisha ya wanaokusanya taka na kuhakikisha kuwa awali yo yote hawapati madhara yoyote.**

Mamilioni ya watu kutoka kote duniani hupata kipato kutokana na kukusanya, kutenga, kutumia tena na kuuza bidhaa ambazo mtu mwingine alikuwa ametupa. Kati nchi nyingine na baadhi ya sehemu mashambani wanaokusanya taka wanabuni tu kundi la kukusanya taka halisi kama vile kinyesi kwa manispaa na inatumiwa tena na kusambaza faida kwa umma na kufikia viwango vikubwa vya matumizi upya. Wanaokusanya taka wanachangia uchumi wa mashinani hadi kwa afya ya umma na usalama pamoja na uendelevu wa mazingira. Ingawa wanatambuliwa katika baadhi ya sehemu bado hadhi yao inachukuliwa kuwa ya chini kwa misingi ya kazi wanayofanya, rangi yao, tabaka n.k maisha yao ni duni na mazingira magumu ya kazi na hupata msaada mdogo sana kutoka kwa serikali za mitaani. Wanazidi kupata changamoto zaidi kutokana na ubinafsishaji wa mifumo ya usimamizi wa taka. Ni vizuri kuwapa taswira zaidi wanaokusanya taka na wafanyikazi wengine katika sekta za jua kali na mashirika na kutambua hadhi zao za msingi za kibinadamu na mchango wao wa kihistoria na kazi wanayofanya wakati huu.

Mabadiliko ya haki katika sekta ya taka ina maana ya kupunguza hewa ya methani kwa njia iliyo sawa na kuhusisha kila mmoja. Inatakiwa kuelekeza jamii kwa mazingira endelevu ya uchumi, ikijumuisha sifa za kazi inayoheshimwa na wote, jamii kuhusishwa, utunzaji wa jamii, fursa zaidi za mafunzo, mabadiliko yanayohitajika ya teknolojia, msaada kwa muundo msingi na kuwapanga wafanyikazi, ulinzi wa kutosha kwa wanaokusanya taka na wanaofanya kazi katika sekta ya taka. Utaratibu wa mabadiliko ya haki unatakiwa kusisitiza kuwasaidia wanaokusanya taka na wafanyikazi wengine ambao wamo katika hatari ya kikazi kutokana na mabadilko ya usimamizi wa taka na mabadiliko ya tabia-nchi.

Ni dhahiri, usimamizi wa taka unatakiwa kutambuliwa kama huduma ya msingi kwa umma ambayo inatakiwa kulindwa na serikali. Sera zinatakiwa kulenga kilele cha fursa za kijamii na kiuchumi za kumaliza uharibifu wa hewa huku changamatoto zozote zikipunguzwa na kusimamiwa kwa makini – ikijumuisha mazungumzo bora kwa jamii kati ya makundi yote ambayo yameguswa, na kuheshimu haki za msingi za binadamu.

Serikali ama serikali za mitaa zinatakiwa kuzingatia mbinu zifuatazo:

- **Kutokana na kuwa washikadau wengi katika mfumo wa taka wamo katika hatari, wanaokusanya taka wanatakiwa kutajwa na kutambuliwa kwa dhati, hivyo taratibu za kisheria zinatakiwa kuzingitiwa : Azimio la pamoja kuhusu Haki za Binadamu, FPIC, UNDRIP (Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu watu asilia) na kadhalika, na mikataba mingine muhimu kama vile ya shirika la Ulimwengu la ILO kuhusu wafanyikazi wasiohudumu katika mazingira rasmi ambao wanakusanya taka na kutumia upya taka.**
- **Kutambua mbinu ya kuhakikisha usawa, kuhusishwa na mabadiliko ya haki kwa wanaokusanya taka na wafanyikazi wengine ambavyo wameathiriwa mifumo ya vipindi vya kazi na sera katika nchi zote — si tu katika nchi zinazoendelea.**
- **Kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyikazi katika sekta ya taka na wanaokusanya taka na kuwathamini, hii inajumuisha kuwatambua kisheria na kuwasaidia wanaokusanya taka katika mazingira yasiyo rasimi, kufikia huduma za afya, elimu na usalama.**
- **Kuboresha dhima ya wanaokusanya taka katika mfumo wa kuongeza thamani na kuendeleza mzunguko wa uchumi kwa kuanisha ushirikiano na wanaokusanya taka (miungano, ushirika na waliojiajiri wenyewe) kwa kukomboa taka inayotoka kwa wanyama na mimea kupitia kwa mabadiliko ya miradi.**
